



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.MZA/KDC/S.10/40/42

24 Mei, 2022

### YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na Dereva Daraja la II**. Tangazo hili ni kutokana na kibali cha Ajira chenye Kumb.Na.FA.97/228/01/9 cha tarehe **13/05/2022** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

#### 1. MTENDAJI WA KIJJI DARAJA LA III – NAFASI (14)

##### 1.1 SIFA ZA MWOMBADI

Mwombaji anatakiwa awe mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (Form Six) aliyehitimu astashahada/cheti (**NTA LEVEL 5**) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### 1.2 MAJUKUMU

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- II. Kusimamia mapato na matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- III. Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- IV. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- V. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- VI. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- VII. Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo laki na kuhamasisiha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VIII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- IX. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

##### 1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali yaani TGS B.

Uk. 1

## **2. DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 4**

### **2.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na ufaulu/Cheti cha kidato cha Nne na Leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundı Stadi (VETA) AU Chuo kingine kinachotambulika na Serikali. Waombaji wenge Cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### **2.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- II. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- III. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- IV. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- V. Kuja za kutunza taarifa za safari zote katika Daftari la Safari
- VI. Kufanya usafi wa gari.
- VII. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

### **2.3 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali yaani TGS B.

## **3.0 MASHARTI YA JUMLA**

- I. Waombaji wawe ni Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
- II. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenyne Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- III. Waombaji wawasilishe picha ndogo mbili za hivi karibuni (passport size).
- IV. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha "Result Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcripts HAVITAKUBALIKA".
- V. Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- VI. Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka 'NACTE'
- VII. Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio watakaoitwa katika usaili.
- VIII. Waombaji waandike namba ya Kitambulisho cha Taifa katika barua zao za maombi ya kazi au waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- IX. Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
- X. Waombaji wenge mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao.
- XI. Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
- XII. Maombi yatakayoletwa moja kwa moja bila kupitia Posta hayatafanyiwa kazi.
- XIII. **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 07 Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri.**  
**Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta tu kwa Anuani ifuatayo:**

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya.  
S.L.P. 88,  
NGUDU-KWIMBA.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovoti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba  
[www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)

Tangazo hili limetolewa na:

H.J. Msanga,  
**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YAKWIMBA**